HOTUBA YA MHE. RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, KATIBA UZINDUZI WA JENGO LA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA LILILOKO ENEO LA MAZIZINI TAREHE 6 OKTOBA 2015

Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais,

Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais;

Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Waziri wa Katiba na Sheria;

Mheshimiwa Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar;

Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho, Spika wa Baraza la Wawakilishi;

Waheshimiwa Mawaziri;

Mheshimiwa Abdalla Mwinyi, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi;

Mhe. Balozi Mdogo wa China,

Waheshimiwa Makatibu Wakuu;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Asalaam Aleykum

Awali ya yote, nianze hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na utukufu kwa kutuajaalia afya njema na uhai tukaweza kukutana katika shughuli yetu hii adhimu.

Ninajisikia faraja na furaha kubwa kuungana nanyi katika hafla hii ya ufunguzi rasmi wa jengo jipya la Wizara ya Katiba na Sheria, ujenzi ambao umegharamiwa na Serikali yetu ya Mapinduzi kwa asilimia mia moja. Hili ni jambo la kujivunia.

Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Kazi ya Ujenzi wa Jengo hili ni matokeo ya mikakati thabiti ya Serikali yetu katika kuimarisha mazingira ya utoaji wa huduma kwa wananchi wetu. **Imeelezwa kuwa jengo hili ni la ghorofa saba na lina ghorofa moja ya chini ya ardhi "basement" ambayo itatumika kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu na nyaraka mbalimbali za taasisi za Wizara.** Tumeambiwa pia kuwa jengo hili kwa sasa limekusanya Idara saba; sita za Wizara ya Katiba na Sheria na moja ya Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati; kama ifuatazo:- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana; Wakala wa wa Usajili Biashara na Mali; Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo**;** Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki, na Ofisi ya Msajili wa Ardhi. Nimeelezwa pia kuwa taasisi hizo zina jumla ya wafanyakazi 223 ambao wamo

ndani ya jengo hili. Hii ni fikra njema inayosaidia kufanya matumizi bora ya ardhi na ifaayo kuendelezwa. Katika kuendeleza fikra hiyo, Serikali sasa ina mpango wa kujenga jengo moja kisiwani Pemba ambalo litatumiwa na wizara tatu. Imeelezwa pia kuwa jengo hili linahudumia watu 200 hadi 450 kwa siku. Ni wazi kuwa changamoto zilizotokana na uchakavu na ufinyu wa nafasi za ofisi zilizokuwa katika jengo la Mambo Msiige na baadaye jengo la zamani la Benki ya Watu wa Zanzibar zimepatiwa ufumbuzi. Hakika hii ni hatua nzuri katika juhudi za kutatua kero za wananchi.

Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Uzinduzi wa jengo hili unaweka ushahidi mwingine wa maendeleo endelevu yaliyoletwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kujenga majengo ya kisasa yenye mvuto na yanayoendana na mahitaji ya wakati huu. Vile vile ni utekelezaji wa azma ya Serikali yetu ya kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi. Azma hii imeelezwa bayana katika Mkakati wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma, ulioandaliwa mwaka 2010 kupitia Eneo la Pili la Kimkakati linaloazimia, pamoja na mambo mengine, kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi ya watumishi wa umma. Kwa hakika mazingira ya jengo hili ni mazuri na yanavutia. Ni matumaini yangu kuwa wafanyakazi mliomo kwenye jengo hili mtayatumia mazingira bora na huduma za kisasa zilizomo katika jengo kama

chachu ya kuimarisha utendaji kazi na hivyo kuleta ufanisi zaidi katika kuwahudumia wananchi.

Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Jengo hili nililolizindua leo linaandika historia nyengine ya mafanikio yaliyopatikana katika Awamu ya Sita ya Uongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sina shaka mtakubaliana nami kuwa haiba ya mji wetu wa Zanzibar inaendelea kubadilika kila uchao kutokana na kuongezeka kwa majengo yanayovutia likiwemo jengo hili. Muonekano wa jengo hili katika Barabara kubwa iendayo Uwanja wa Ndege unavutia wengi, wakiwemo wageni wetu wanaokuja Zanzibar kwa shughuli mbalimbali na hata Watalii. Katika eneo hili la Mazizini tayari yapo majengo ya Serikali yenye hadhi ya kileo ambayo ni Wizara ya Elimu, Bodi ya Mapato Zanzibar na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Nimefurahi kusikia kuwa tayari mmeandaa mpango endelevu wa kulitunza jengo hili. Ni matumaini yangu kuwa wafanyakazi pamoja na wananchi wanaokuja kupata huduma, mtashiriki vyema kulitunza na kulienzi jengo hili ili lidumu na liendelee kuwa kivutio cha mji wetu.

Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Haiba ya Jengo hili itakamilika pale ambapo tutalipa jina muafaka litakaloweka kumbukumbu nzuri kulingana na matumizi yake. Ni kwa mnasaba huo jengo hili tunalipa jina la **.....**".

Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza CRJE-East Africa, Kampuni ya Ujenzi wa jengo hili kwa kazi nzuri waliyoifanya. Aidha ninawapongeza NEDCO, Mshauri wa Ujenzi wa jengo hili kwa usimamizi wao thabiti. Vile vile ninawapongeza Watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali zilizochangia kufanikisha utekelezaji wa mradi huu, kwa kutoa ushauri na maelekezo ya kitaalamu, kila yalipohitajika na hatimaye kufikia hatua hii. Hongereni sana.

Namalizia hotuba yangu kwa kuwakumbusha wananchi wote kwa ujumla kuwa zimebakia siku chache tu kuelekea siku ya Uchaguzi Mkuu. Kila mwananchi aliyetimiza masharti anatakiwa kwenda kupiga kura kuchagua viongozi watakaoongoza nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Hii ni fursa adhimu ya kidemokrasia inayomuwezesha kila mmoja wetu kushiriki kuwaweka madarakani viongozi bora watakaoiletea maendeleo nchi yetu.

Ndugu Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Sina budi kwa mara nyengine kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuifanya shughuli yetu hii kwa mafanikio.

Asanteni kwa kunisikiliza.